Kadi Rahisi ya Alama za Umaskini
Simple Poverty Scorecard®
Tanzania

Mark Schreiner

27 Juni 2016

This document and related tools are in English at `SimplePovertyScorecard.com`
Hati hii na zana husika zimo kwa lugha ya Kiswahili kwenye `SimplePovertyScorecard.com`

Muhtasari

Kadi Rahisi ya Alama za Umaskini inatumia viashiria kumi vya gharama za chini kutoka kwenye Utafiti wa Bajeti za Kaya wa mwaka wa 2011/12 wa Tanzania ili kukadiria uwezekano kwamba kaya ina matumizi ya chini ya mstari fulani wa umaskini. Wafanyakazi wa uwandani wanaweza kukusanya majibu kwa takriban dakika kumi. Usahihi umeripotiwa kwa mistari mbali mbali ya umaskini. Kadi ya alama ni njia fanisi kwa mipango ya kuwasaidia maskini nchini Tanzania ya kupima viwango vya umaskini, ili kufuatilia mabadiliko katika viwango vya umaskini baada ya muda, na ili kuainisha wateja kwa ajili ya huduma lengwa.

Dokezo la toleo

Hati hii inatumia data ya mwaka wa 2011/12, na kuchukua mahali pa Schreiner (2013a), ambayo inatumia data ya 2007. Kadi mpya ya alama ya mwaka wa 2011/12 hapa inafaa kutumia kuanzia sasa. Kadi hizi mbili za alama *hazitumii* ufafanuzi sawia wa *umaskini*, kwa hivyo hakuna njia halali kwa watumizi wa sasa wa Schreiner (2013a) kupima badiliko baada ya muda wakitumia msingi kutoka kwenye kadi ya zamani ya alama ya mwaka wa 2007 na ufuatiliaji kutoka kwenye kadi mpya ya alama ya mwaka wa 2011/12.

Shukrani

Hati hii ilifadhiliwa na Grameen Foundation (GF). Tafsiri ya Kiingereza hadi Kiswahili iliyofanywa na George Karanja (`mail@georgekaranja.com`) ilifadhiliwa na Microfinance Risk Management, L.L.C. Data zimetolewa kwenye Ofisi ya Taifa ya Takwimu ya Tanzania. Shukrani zimwendee Julie Peachey, Sharada Ramanathan, na Sasun Tsirunyan. Kadi Rahisi ya Alama za Umaskini pia inajulikana kama Progress out of Poverty Index®. GF inasimamia na kukuza PPI® kama zana ya kusaidia mashirika kupima umaskini wa washiriki wake ili kufanikisha malengo yao ya kijamii kwa ufanisi zaidi. Nyenzo na rasilimali za mafunzo za PPI zimo kwenye `progressoutofpoverty.org`. Copyright © 2017 by Mark Schreiner. All rights reserved.

Mwandishi

Mark Schreiner ni mkurugenzi wa Microfinance Risk Management, L.L.C. Pia yeye ni Senior Scholar katika Center for Social Development cha Washington University in Saint Louis.

Kadi Rahisi ya Alama za Umaskini
Simple Poverty Scorecard®

			Jina	Kitambulishi
Na. ya mahojiano:				
Tarehe ya mahojiano:		Mshiriki:		
Nchi:	TZA	Ajenti wa uwandani:		
Kadi ya alama:	002	Kituo cha huduma:		
Sampuli ya uzani:		Idadi ya jamaa wa kaya:		

Kiashiria	Jibu	Alama	*Score*
1. Ni jamaa wangapi wa kaya wana umri wa miaka 18 au chini?	A. Sita au zaidi	0	
	B. Watano	2	
	C. Wanne	5	
	D. Watatu	11	
	E. Wawili	14	
	F. Mmoja	17	
	G. Hakuna	28	
2. Jamaa wote wa kaya wenye umri wa miaka 6 hadi 18 wanaenda shule hivi sasa?	A. La	0	
	B. Ndio	3	
	C. Hakuna jamaa wa umri wa miaka 6 hadi 18	5	
3. Kuta za jengo kuu zimejengwa kwa nyenzo ipi?	A. Matofali yaliyookwa	0	
	B. Vigingi na matope, nyasi, matofali yaliyokaushwa kwa jua, au nyingine	6	
	C. Mawe, matofali ya saruji, au mbao	13	
4. Paa ya jengo kuu limejengwa kwa nyenzo ipi?	A. Nyasi/matawi. Matope na matawi, au nyingine	0	
	B. Mabati, matofali, saruji, au asbesto	6	
5. Aina kuu ya moto unaotumiwa kwa mapishi ni upi?	A. Kuni, makaa ya mawe, miale ya jua, gesi (bayogesi), kuni/mabaki ya shambani, au kinyesi cha wanyama	0	
	B. Makaa, mafuta taa, gesi (ya viwandani), stima, jenereta/chanzo cha kibinafsi, au nyingine	9	
6. Kaya yako ina televisheni zozote?	A. La	0	
	B. Ndio	15	
7. Kaya yako ina redio, vifaa vya kaseti/ kanda, au vifaa vyovyote vya hi-fi?	A. La	0	
	B. Ndio	4	
8. Kaya yako ina taa zozote?	A. La	0	
	B. Ndio	4	
9. Kaya yako ina meza zozote?	A. La	0	
	B. Yes	4	
10. Ikiwa kaya ilikuza mimea yoyote katika miezi 12 iliyopita, kwa sasa inamiliki ng'ombe dume, ng'ombe kike, ng'ombe dume aliyehasiwa, mori, ndama wa kiume, ndama wa kike, au ng'ombe maksai wowote?	A. Hakuna mimea, na hakuna ng'ombe	0	
	B. Hakuna mimea, na ng'ombe wako	0	
	C. Mimea, lakini hakuna ng'ombe	5	
	D. Mimea, na ng'ombe	12	

***Score*:**

Lahakazi ya Ukurasa wa Nyuma:
Jamaa wa Kaya, Umri, na Kuenda Shule

Katika kichwa cha kadi ya alama, andika kitambulishi cha kipekee cha mahojiano (ikwa kinajulikana), tarehe ya mahojiano, na sampuli ya uzani wa mshiriki (ikiwa unajulikana). Kisha rekodi majina na nambari za utambulisho za kipekee za mshiriki (ambaye anayeweza kuwa tofauti na mhojiwa), zako kama ajenti wa uwandani, na za kituo cha huduma ambacho mshiriki anatumia.

Muulize mhojiwa: *Tafadhali nieleze jina na umri wa kila jamaa wa kaya hii.* Kaya *ni mtu mmoja au kundi la watu—bila kujali uhusiano wa damu au ndoa—ambao kwa kawaida wanaishi pamoja katika makazi moja, wanakula pamoja, na wanaleta rasilimali zao pamoja. Tafadhali anzia na kiongozi wa kaya.*

Katika kichwa eneo la "Idadi ya jamaa wa kaya", rekodi idadi ya jamaa (bila kujali umri).

Katika jedwali lililo hapo chini, weka alama kana kwamba kila jamaa wa kaya ana umri wa miaka 18 au chini. Hesabu ni wangapi wana umri wa miaka 18 au chini na uweke alama kwenye jibu la kiashiria cha kwanza cha kadi ya alama.

Kisha weka alama kana kwamba kila jamaa wa kaya ana umri wa kati ya miaka 6 hadi 18. Kwa kila jamaa katika umri huu, uliza: "<jina> kwa sasa anaenda shule?" na uweke alama kwenye jibu hilo. Kisha kagua kana kwamba jamaa wote walio na umri wa kati ya miaka 6 hadi 18 wanaenda shule (au kana kwamba kuna jamaa wowote walio katika umri huu) na uweke alama kwenye jibu la kiashiria cha pili cha kadi ya alama.

Kumbuka ufafanuzi kamili wa *kaya* katika "Miongozo ya Fasiri ya Viashiria vya Kadi ya Alama".

Jina	**Umri**	**≤ 18?**	**≥ 6 and ≤ 18?**	**<jina> kwa sasa anaenda shule?**
1.		La Ndio	La Ndio	Hana miaka 6 hadi 18 La Ndio
2.		La Ndio	La Ndio	Hana miaka 6 hadi 18 La Ndio
3.		La Ndio	La Ndio	Hana miaka 6 hadi 18 La Ndio
4.		La Ndio	La Ndio	Hana miaka 6 hadi 18 La Ndio
5.		La Ndio	La Ndio	Hana miaka 6 hadi 18 La Ndio
6.		La Ndio	La Ndio	Hana miaka 6 hadi 18 La Ndio
7.		La Ndio	La Ndio	Hana miaka 6 hadi 18 La Ndio
8.		La Ndio	La Ndio	Hana miaka 6 hadi 18 La Ndio
9.		La Ndio	La Ndio	Hana miaka 6 hadi 18 La Ndio
10.		La Ndio	La Ndio	Hana miaka 6 hadi 18 La Ndio
11.		La Ndio	La Ndio	Hana miaka 6 hadi 18 La Ndio
12.		La Ndio	La Ndio	Hana miaka 6 hadi 18 La Ndio
13.		La Ndio	La Ndio	Hana miaka 6 hadi 18 La Ndio
# Jamaa:		**#≤18:**	—	**#La:** **#Ndio:**

Tazama jedwali ili kugeuza alama kuwa uwezekano wa umaskini: Mistari ya umaskini ya taifa

	Uwezekano wa Umaskini (%)			
	Mistari ya umaskini ya kitaifa			
Score	**Chakula**	**100%**	**150%**	**200%**
0–4	100.0	100.0	100.0	100.0
5–9	39.5	100.0	100.0	100.0
10–14	36.6	82.3	93.1	100.0
15–19	29.9	62.1	89.2	98.6
20–24	21.0	51.2	84.5	93.8
25–29	13.3	40.3	77.4	93.8
30–34	10.4	32.9	68.0	87.4
35–39	4.4	20.2	58.1	79.4
40–44	2.8	14.0	42.5	67.9
45–49	1.5	10.9	40.2	63.7
50–54	1.3	6.6	29.2	51.2
55–59	0.6	4.1	24.2	43.8
60–64	0.6	2.2	13.5	31.8
65–69	0.4	1.3	8.6	28.1
70–74	0.0	1.0	5.9	19.5
75–79	0.0	1.0	5.9	16.8
80–84	0.0	1.0	2.6	7.3
85–89	0.0	0.0	2.2	7.3
90–94	0.0	0.0	0.0	7.3
95–100	0.0	0.0	0.0	0.0

Tazama jedwali ili kugeuza alama kuwa uwezekano wa umaskini: Mistari ya umaskini ya PPP ya mwaka wa 2005 na 2011 ya kimataifa

	Uwezekano wa Umaskini (%)							
	Mistari ya umaskini ya PPP ya 2005				Mistari ya umaskini ya PPP ya 2011			
Score	**$1.25**	**$2.00**	**$2.50**	**$5.00**	**$1.90**	**$3.10**	**$3.80**	**$4.00**
0–4	100.0	100.0	100.0	100.0	100.0	100.0	100.0	100.0
5–9	100.0	100.0	100.0	100.0	100.0	100.0	100.0	100.0
10–14	86.7	100.0	100.0	100.0	89.0	100.0	100.0	100.0
15–19	77.5	99.9	99.9	100.0	85.0	99.9	99.9	99.9
20–24	71.9	93.0	97.0	99.7	78.0	96.3	97.4	98.3
25–29	59.6	92.4	96.7	99.5	70.6	94.5	97.4	98.0
30–34	48.0	84.3	95.0	99.5	57.7	91.7	96.7	97.7
35–39	35.2	77.2	89.5	99.5	47.2	84.4	92.5	94.1
40–44	23.5	64.3	79.6	98.5	31.2	71.8	85.4	88.9
45–49	20.2	54.3	75.7	97.3	28.5	66.1	81.8	84.1
50–54	13.8	45.4	61.2	94.2	18.8	54.0	69.7	72.2
55–59	7.3	38.7	56.9	93.4	11.9	45.5	63.1	65.3
60–64	4.2	25.1	45.6	86.1	5.8	33.7	50.2	53.8
65–69	1.7	21.3	36.8	79.9	3.7	28.9	44.7	46.8
70–74	1.7	13.8	27.1	78.7	3.1	21.2	34.4	37.2
75–79	1.7	12.8	23.2	71.3	2.9	20.1	33.0	35.7
80–84	1.3	3.1	8.1	44.2	1.3	6.3	11.4	13.4
85–89	0.1	2.8	8.1	38.3	1.2	6.3	11.4	13.4
90–94	0.0	0.0	7.6	30.6	0.0	6.3	7.6	7.6
95–100	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0

Tazama jedwali ili kugeuza alama kuwa uwezekano wa umaskini: Mistari ya umaskini husiani na yenye msingi wa asilimia

	Uwezekano wa Umaskini (%)					
	Nusu maskini zaidi	Mistari kwa msingi wa asilimia				
Score	**<100% Natl.**	**Ya 20**	**Ya 40**	**Ya 50**	**Ya 60**	**Ya 80**
0–4	100.0	100.0	100.0	100.0	100.0	100.0
5–9	80.6	100.0	100.0	100.0	100.0	100.0
10–14	49.2	76.6	89.0	90.1	98.6	100.0
15–19	42.6	53.2	78.8	88.1	95.0	99.9
20–24	25.6	38.3	71.8	80.1	87.6	97.1
25–29	20.6	28.0	58.0	73.7	83.9	96.9
30–34	16.9	23.2	48.4	60.8	74.2	95.4
35–39	8.1	12.5	36.3	48.9	62.4	88.0
40–44	5.4	7.9	23.2	33.0	45.4	80.4
45–49	3.1	5.4	17.9	27.4	39.4	72.4
50–54	1.7	3.4	12.1	17.6	26.8	54.6
55–59	0.5	0.6	6.0	8.6	18.8	46.4
60–64	0.5	0.6	1.8	4.4	10.3	33.0
65–69	0.3	0.4	1.1	1.3	5.5	22.7
70–74	0.0	0.0	1.1	1.3	2.6	13.9
75–79	0.0	0.0	1.0	1.3	2.6	12.8
80–84	0.0	0.0	0.0	1.3	1.4	5.3
85–89	0.0	0.0	0.0	0.1	0.1	5.3
90–94	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
95–100	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0

Miongozo ya Fasiri ya Viashiaria vya Kadi ya Alama

Dondoo zilizonukuliwa hapo chini zimetolewa kwenye:

National Bureau of Statistics. (2011) "Instruction Manual: Household Budget Survey, 2011/12", [*Mwongozo*], `catalog.ihsn.org/index.php/catalog/4846/download/60555`, ilirejeshwa mnamo tarehe 3 Juni 2016.

na

National Bureau of Statistics. (2011) "Questionnaire: Household Budget Survey, 2011/12", [*Hojaji*], `nbs.go.tz/nbs/takwimu/hbs/201-12_HBS_Technical-Report.zip`, ilirejeshwa mnamo tarehe 3 Juni 2016..

Mwongozo wa nchi ya Tanzania sio kawaida kuwa bila taarifa muhimu. Kama inavyotendeka mara nyingi, wakati suala linaibuka ambalo halijaangaziwa hapa, suluhu yake inafaa kuachiwa uamuzi bila kusaidiwa wa anayefanya sensa, kwani yaonekana kama hiyo ndiyo ilikuwa hatua ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu ya (NBS) katika HBS ya mwaka wa 2011/12. Yaani, shirika linalotumia Kadi Rahisi ya Alama za Umaskini halifai kutangaza fafanuzi wala sharia zozote (isipokuwa zile ziko katika "Miongozo" hii) kutumiwa na maajenti wake wote wa uwandani, Chochote ambacho hakijaangaziwa katika "Miongozo" hii kinafaa kuachiwa uamuzi bila kusaidiwa wa kila anayefanya sensa.

Kwa kukubali, hii sio njia ya kuridhisha ya kutatua masuala hayo, lakini bila ufahamu (kutoka kwa chanzo kingine kando na *Mwongozo*) wa kile ambacho NBS iliwafunza wanaofanya sensa kufanya katika HBS ya 2011/12, hakuna mbadala bora zaidi.

Miogozo jumla ya kuuliza maswali ya kadi ya alama

Jaza kichwa cha kadi ya alama na "Lahakazi ya Ukurasa wa Nyuma" kwanza, kwa kufuata maelekezo yaliyo kwenye "Lahakazi ya Ukurasa wa Nyuma".

Usiulize kiashiria cha kwanza cha kadi ya alama moja kwa moja ("Ni jamaa wangapi wa kaya wana umri wa miaka 18 au chini?"). Badala yake, tumia taarifa iliyorekodiwa kwenye "Lahakazi ya Ukurasa wa Nyuma" ili kujua ni jibu lipi utakaloweka alama. Pia ni lazima urekodi idadi ya jamaa wa kaya (bila kujali umri) katika kichwa cha kadi ya alama karibu na "Idadi ya jamaa wa kaya"

Vivyo hivyo, usiulize kiashiria cha pili moja kwa moja ("Jamaa wote wa kaya wenye umri wa miaka 6 hadi 18 kwa sasa wanaenda shule?"). Badala yake, tumia taarifa iliyorekodiwa kwenye "Lahakazi ya Ukurasa wa Nyuma" ili kujua ni jibu lipi utakaloweka alama.

Kwa jumla, usimsomee mhojiwa chaguo za majibu. Soma tu swali, na kisha uache; subiri jibu. Mhojiwa akiomba ufafanuzi au vinginevyo akisita au aonekane kukanganywa, basi soma swali tena na umpe usaidizi wa ziada kimsingi na "Miongozo" hii au kama vile wewe, mfanya sensa, unavyoona mwafaka.

Kwa jumla, unafaa kukubali majibu yanayopeanwa na mhojiwa. Hata hivyo, mhijiwa akisema kitu—au ukiona au uhisi kitu—ambacho kinadokeza kwamba jibu huenda likawa sio sahihi, kwamba mhojiwa hana uhakika, au kwamba mhojiwa angependa kupata usaidizi ili kuelewa jinsi ya kujibu, basi unafaa kusoma swali hilo tena na kumpa usaidizi wowote ule unaoona kwamba unafaa kimsingi na "Miongozo" hii.

Ingawa viashiria vingi katika Kadi Rahisi ya Alama za Umaskini vinaweza kuthibitishwa, kwa jumla, hauhitaji kuthibitisha majibu. Unafaa kuthibitisha jibu ikiwa tu kuna kitu kinachokudokezea kwamba jibu hilo huenda sio sahihi na kwa hivyo uthibitishaji unaweza kuboresha ubora wa data.

Kwa mfano, unaweza kuchagua kuthibitisha mhojiwa akisita, au akionekana mwenye wasiwasi, au vinginevyo akitoa ishara kwamba huenda anadanganya au amekanganyika. Vivyo hivyo, uthibitishaji huenda ukawa mwafaka ikiwa mtoto katika kaya hiyo au jirani akisema kitu ambacho hakilingani na jibu la mhojiwa.

Uthibitishaji pia ni dhana nzuri ukiona kitu wewe mwenyewe—kama vile kifaa ambacho mhojiwa anadai kuwa hamiliki, au mtoto akila chumbani kingine ambaye hajahesabiwa kama jamaa wa kaya hiyo—hilo linadokeza kwamba huenda jibu sio sahihi.

Kwa jumla, utumizi wako wa Kadi Rahisi ya Alama za Umaskini unafaa kuiga kwa karibu iwezekanavyo utumizi wa NBS wa HBS ya 2011/12. Kwa mfano, mahojiano ya kuwekea umaskini alama yanafaa kufanyika katika boma za wahojiwa kwa sababu HBS ya 2011/12 ilifanyika katika boma za wahojiwa.

Tafsiri ya Hojaji:

Inaonekana kwamba HBS ya 2011/12 iliachia kila mfanya sensa binafsi kufanya tafsiri ya zana ya utafiti kwa lugha nyingine kando na Kiingereza (pengine kwa usaidizi wa watafsiri wenyeji). Wakati tafsiri hiyo ilipohitajika, ilifanywa kwa haraka.

Ingawa utumizi wa Kadi Rahisi ya Alama za Umaskini, kwa jumla, inafaa kuiga utumizi wa HBS ya 2011/12, hata hivyo ni muhimu kuwa na tafsiri wastani, iliyofanywa vizuri, na kukaguliwa kwa lugha ambazo zinatumika zaidi nchini Tanzania (kama vile Kiswahili, kati ya zingine).

Bila tafsiri wastani, tofauti katika tafsiri na fasiri za wanaofanya sensa inaweza kudhuru pakubwa ubora wa data. Bila shaka, tafsiri yoyote inafaa kuonyesha maana haswa katika zana asilia ya utafiti wa HBS ya Kiingereza, mashirika yote yanayotumia kadi ya alama katika lahaja au lugha fulani nchini Tanzania zinaweza kushirikiana ili kutengeneza na kutumia tafsiri moja.

Faragha:

Kulingana na ukurasa wa kichwa wa *Hojaji*, taarifa yote iliyokusanywa "ni ya faragha kikiki na itatumiwa kwa dhumuni la kitakwimu pekee."

Kulingana na uk. 2 wa *Mwongozo*, "Weka taarifa iliyokusanywa faraghani kikiki. Usiifichue kwa mtu yeyote isipokuwa wale waliohusika katika utafiti. Waeleze wahojiwa kwamba taarifa yao itaunganishwa na kusanidiwa ili kuunda ripoti ya kitakwimu. Wahakikishie wahojiwa kwamba taarifa hiyo itawekwa faraghani na itatumiwa tu wa madhumuni ya kitakwimu."

Ni nani anafaa kuwa mhojiwa?

Kulingana na uk. 4 wa *Mwongozo*, "Ikiwa kiongozi wa kaya hapatikani, basi jamaa yeyote mwingine wa kaya anaweza kuhojiwa." Hii inaonyesha kwamba mhojiwa anayependelewa zaidi ni kiongozi wa kaya.

Kulingana na uk. 14 wa *Mwongozo*, *kiongozi wa kaya* ni "mtu anayetambuliwa kama kiongozi na jamaa wengine wote wa kaya. Mara nyingi anawajibikia kutafuta fedha na maslahi ya jamaa wa kaya."

<u>Vitu vya kubeba</u>:
Kulingana na uk. 5 wa *Mwongozo*, unafaa kubeba vitu vifuatavyo ukienda kwenye mahojiano:

- Kitambulisho chako
- Barua ya utangulizi kutoka kwa [shirika lako]
- [“Miongozo” hii]
- Orodha ya kaya utakazohoji
- Nakala za [kadi ya alama]

<u>Sanaa ya kuhoji</u>:

<u>Kukutana na kaya kwa mara ya kwanza</u>
Kulingana na uk. 7 wa *Mwongozo*, “Tabia na mtazamo wako ni muhimu sana. Kama mhoji, jukumu lako la kwanza ni kuunda uhusiano mwema. Mwanzoni mwa mahojiano, wewe na mhojiwa hamjuani. Mwonekano wako wa kwanza na mhojiwa utaadhiri hali yake ya kuwa tayari kushirikiana nawe. Kuwa wa kirafiki inapojiwasilisha kwake kwa mara ya kwanza.

“Beba barua na kitambulisho zinazoonyesha kwamba unafanya kazi na [shirika lako].

“Kumbuka kuvalia mavazi ya kuheshimika. Wanawake wanafaa kuvalia kanga au kitenge ili kujikinga, kwani sio kaya zote zina viti.”

<u>Jukumu lako kama mfanya sensa</u>
Kulingana na uk.7–8 wa *Mwongozo*, “Una jukumu kuu zaidi katika utafiti. Kama mfanya sensa, jukumu lako ni kukusanya data inayohitajika. Ubora wa kazi yako unaamuliwa na ubora wa data unayokusanya. Hatima ya utafiti inakutegemea wewe.

“Kwa uangalifu fuata [maagizo haya].

“Unda hali ya kirafiki na mhojiwa ili uweze kupata data sahihi. Kuunda hali ya kuaminiana kunasaidia, na pia kunakusaidia wewe kufahamu utamaduni na tabia za jamii unayofanya kazi nayo.

“Mwonekano wako na maneno na hatua zako za kwanza ni muhimu sana kwa kujishindia ushirikiano wa mhojiwa.

“Washawishi wahojiwa kwamba wewe ni mwenye maarifa na kwamba ushiriki wao katika zoezi la utafiti utanufaisha [washiriki wa shirika lako].

“Usitajie—wala kuahidi—kaya inayohojiwa (wala mtu yeyote mwingine) manufaa yoyote ya papo hapo yatakayotokana na utafiti huo, kwani hili linaweza kuathiri majibu.

“Taja hali ya faragha ya majibu. Fanya mahojiano wewe na mhojiwa pekee yenu.

“Fanya mahojiano kuwa mafupi, lakini usimharakishe mhojiwa.

“Tofauti na mazungumzo ya kawaida, katika mahojiano unauliza maswali yote, naye mhojiwa anapeana majibu yote. Usiwahi kutoa maoni yako, na usitoe hisia zako kwa njia yoyote kuhusiana na kile mhojiwa anachokisema. Usionyeshe kukubaliana wale kukataana na kitu chochote; nyakati zote usiegemee upande wowote.

“Ikiwa mhojiwa anasita au hayuko tayari kujibu swali Fulani, basi jaribu kukabiliana na hilo. Elezea kwamba taarifa zote ni za faragha. Lakini usimsisitizie sana akupe jibu; mhijiwa hawezi kulazimishwa kujibu maswali.

“Fuata mfuatano wa maswali kikiki kama yaliyoandikwa.” Yasome neo kwa neo kama yalivyoandikwa. Haswa, usiweke alama kwenye jibu isipokuwa kama umemuuliza mhojiwa swali naye mhojiwa amepeana jibu.

“Dhibiti hali hiyo. Dumisha hamu ya mhijiwa nyakati zote. Mhojiwa akikengeushwa au kuzungumza bila mpangilio, basi usimsitishe ghafla au kwa ufidhuli; sikiliza anachokisema, kisha kwa ungwana ujaribu kumrejesha kwenye swali”

<u>Kushawishi kaya zinazosita</u>

Kulingana na uk. 8–9 wa *Mwongozo*, “Matokeo kutoka kwa tafiti ambako juhudi zaidi zinafanywa ili kushawishi kaya husika kushiriki ni ya uwakilishi zaidi kuliko tafiti ambako ni wahojiwa walio tayari kushiriki pekee wanahojiwa. Kwa mfano, tafiti zinazotumia kaya zinazochukua mahali pa kaya zingine mara nyingi zinawakilisha wazee na watu wanaokaa nyumbani. Kaya zilizo kwenye orodha yako ya sampuli zimechaguliwa bila mpangilio. Haziwezi kubadilishwa kwa kaya zingine.

“Jaribu juhudi zako bora kupata data sahihi. Jaribu kuunda uhusiano mwema na kaya hiyo. Kuwa mwaminifu kwao kila wakati na kuonyesha uaminifu wa kweli. Ikiwa una miadi na kaya hiyo, jaribu kufika pale kwa wakati ambao mlielewana.

“Utakuwa na mtindo wako binafsi wa kushawishi kaya ambayo haiko tayari kushirikiana ili iweze kushirikiana nawe. Mambo muhimu ya kuzingatia ni:

- Ifanye kaya husika kuhisi kwamba ndiyo kaya muhimu zaidi katika utafiti huo. Endesha majibu yako kulingana na hali zao binafsi. Ikiwa wana shughuli nyingi, ni wagonjwa, au wamechokozwa, basi jishughulishe na tatizo lao
- Kuwa tayari kubadilisha mambo kwa urahisi. Ikiwa mhojiwa anataka kubadilisha miadi au anataka umpigie simu wakati mwingine, basi iweke wazi kwamba hauna shida kuwazingatia
- Fanya chochote uwezacho kushawishi kaya kushirikiana nawe
- Hakikisha umeieleza kaya kwamba utafiti huu unanufaisha [washiriki wa shirika lako]
- Kaya bado ikikataa, tafuta usaidizi kutoka kwa kiongozi mwenyeji wa eneo hilo au kutoka kwa msimamizi wako

"Hii ni baadhi ya mikabala fanisi ya kukabiliana na ukataaji:

- Mkumbushe mhojiwa kwamba utafiti huo hauhitajiki kukamilishwa kwa ziara moja na kwamba unaweza kurudi mara nyingi inavyohitajika
- Ikiwa kaya inaogopa kwamba maswali yatakuwa ya kibinafsi sana au ya undani sana, ikumbushe kaya hiyo kuhusu haki yake ya kukataa kujibu maswali binafsi, kwa kusema, 'Mahojiano haya ni ya kujitolea, na tunakutia moyo kukataa maswali ambayo unahisi kuwa ni ya kibinafsi sana, ni nyeti sana, au ni ya undani sana Maswali utakayojibu bado yatakuwa muhimu kwetu, bila kujali ni mangapi'
- Kaya ikidai kwamba ina shughuli nyingi sana, basi sisitiza kwamba ni kundi hili haswa la kaya zenye shughuli nyingi ambalo ni muhimu zaidi kwa utafiti huu. Sema kwamba kwa ajili ya idadi kubwa za watu bila ajira au waliostaafu, unahitaji taarifa zote ambazo wafanyikazi wa muda kamili wanaweza kupeana. Kila wakati iweke wazi kwamba hauna shida kuzingatia mahitajiko yao
- Ikiwa kaya ina wasiwasi kuhusu faragha, wafahamishe kwamba faili hizo zinalindwa kwa maneno msimbo ya siri ambayo yanabadilishwa mara nyingi. Kwa ziada, unaweza kuhakikishia kwamba hakuna taarifa itawahi kupeanwa ambayo inaweza kuhusishwa na jina au anuani yao. Kusisitizia kipengele cha 'hesabu nyingi' cha takwimu mara nyingi husaidia
- Ikiwa kaya ina wasiwasi kwamba, kwa mfano, data yake inaweza kuangukia mikono ya idara za serikali, basi dokeza kwamba takwimu hufichua tu asilimia za idadi badala ya kuchukua kaya yoyote fulani"

Miongozo ya viashiria mahsusi vya kadi ya alama

1. Ni jamaa wangapi wa kaya wana umri wa miaka 18 au chini?
    A. Sita au zaidi
    B. Watano
    C. Wanne
    D. Watatu
    E. Wawili
    F. Mmoja
    G. Hakuna

Ukurasa wa 14 wa *Mwongozo* unafafanua *kaya* kwa orodha ifuatayo ya kauli:

- "Ni jamaa wa kawaida pekee wa kaya wanaweza kuhusika
- Kaya inaweza kuwa na mtu mmoja au zaidi ya mtu mmoja
- *Kaya ya mtu mmoja* ni mtu anayeishi peke yake katika nyumba nzima au sehemu ya nyumba na ambaye na matumizi yake huru
- Kaya ya watu wengi ni kundi la watu wawili au zaidi ambao wanaishi katika nyumba nzima au sehemu yake na ambao anagawana matumizi. Mara nyingi kaya za aina hii zinajumuisha mume, mke, na watoto. Jamaa wengine, wapangaji, na wageni wanazingatiwa kuwa jamaa wa kaya hiyo ikiwa wanaleta rasilimali zao pamoja, wanagawana matumizi, na wamekuwa wakiishi na kaya hiyo kwa angalau wiki mbili
- Watumishi wa kaya wanahesabiwa kama jamaa wa kaya husika ikiwa na ikiwa tu wanakula miloyao pamoja na kaya husika na wanamtambua kiongozi sawia
- Watoto walio katika shule ya bweni wanahesabiwa kama jamaa wa kaya husika
- Wapangaji wanaotumia makazi na milo kwa kulipia wanahesabiwa kama jamaa wa kaya. Mpangaji akikosa kuchangia au hashiriki milo pamoja na jamaa wa kaya, basi mpangaji huyo sio jamaa wa kaya hiyo.
- Mume aliye na wake zaidi ya mmoja anayekaa muda fulani ndani ya zaidi ya kaya moja anahesabiwa kama jamaa wa kaya tu katika kaya ambayo anakaa kwa muda mwingi zaidi.

"Kaya inawajumuisha wale wanaogawana matumizi na wanaoleta rasilimali zao pamoja."

Kulingana na uk. 2 wa *Hojaji*, [wakati unaorodhesha jamaa wa kaya kwenye Lahakazi ya Ukurasa wa Nyuma"] unafaa "kitengeneza orodha kamili ya watu wote ambao kwa kawaida wanaishi na kula milo yao pamoja katika kaya hii, ukianzia na kiongozi wa kaya.

"Ili kuunda orodha ya kina ya jamaa wa kaya:

- Uliza majina na umri wa jamaa wote wa familia ya karibu ambao kwa kawaida wanaishi na kula milo yao pamoja hapa
- Uliza majina na umri wa watu wowote wengine ambao wana uhusiano na jamaa wa kaya na ambao kwa kawaida wanaishi na kula milo yao pamoja hapa
- Uliza majina na umri wa watu wengine ambao hawayuko hapa sasa lakini ambao kwa kawaida wanaishi na kula milo yao hapa (kwa mfano, jamaa wa kaya wanaosomea kwingine au walio safarini)
- Uliza majina na umri wa watu wengine ambao hawana uhusiano na jamaa wa kaya ambao wanaishi na kula milo yao pamoja hapa, kama vile watumishi"

2. Jamaa wote wa kaya wenye umri wa miaka 6 hadi 18 wanaenda shule hivi sasa?
   A. La
   B. Ndio
   C. Hakuna jamaa wa umri wa miaka 6 hadi 18

Mwongozo unatoa taarifa zaidi kuhusiana na kiashiria hiki.

3. Kuta za jengo kuu zimejengwa kwa nyenzo ipi?
    A. Matofali yaliyookwa
    B. Vigingi na matope, nyasi, matofali yaliyokaushwa kwa jua, au nyingine
    C. Mawe, matofali ya saruji, au mbao

Kulingana na uk. 26 wa *Mwongozo*, "Ikiwa nyumba ya kuishi imejengwa kwa kutumia zaidi ya nyenzo moja ya kujengea, basi zingatia nyenzo kuu ya kujengea ambayo ilitumiwa wakati wa mchakato wa ujenzi."

Kulingana na uk. 15 wa *Mwongozo*, *makazi* au *nyumba ya kuishi* ya kaya ni "nafasi yote ya kuishi inayotumiwa na kaya, bila kujali mpangilio wake wa vifaa. Kwa mfano, huenda ikawa ni chumba kimoja kinachotumiwa na wapangaji au huenda ikawa ni nyumba moja, mbili au zaidi zinazotumiwa na familia ya mbali au kaya."

4. Paa ya jengo kuu limejengwa kwa nyenzo ipi?
    A. Nyasi/matawi, matope na matawi, au nyingine
    B. Mabati, matofali, saruji, au asbesto

Kulingana na uk. 26 wa Mwongozo, "Ikiwa nyumba ya kuishi imejengwa kwa kutumia zaidi ya nyenzo moja ya kujengea, basi zingatia nyenzo kuu ya kujengea ambayo ilitumiwa wakati wa mchakato wa ujenzi."

Kulingana na uk. 15 wa *Mwongozo*, *makazi* au *nyumba ya kuishi* ya kaya ni "nafasi yote ya kuishi inayotumiwa na kaya, bila kujali mpangilio wake wa vifaa. Kwa mfano, huenda ikawa ni chumba kimoja kinachotumiwa na wapangaji au huenda ikawa ni nyumba moja, mbili au zaidi zinazotumiwa na familia ya mbali au kaya."

5. Aina kuu ya moto unaotumiwa kwa mapishi ni upi?
    A. Kuni, makaa ya mawe, miale ya jua, gesi (bayogesi), kuni/mabaki ya shambani, au kinyesi cha wanyama
    B. Makaa, mafuta taa, gesi (ya viwandani), stima, jenereta/chanzo cha kibinafsi, au nyingine

Mwongozo unatoa taarifa zaidi kuhusiana na kiashiria hiki.

6. Kaya yako ina televisheni zozote?
    A. La
    B. Ndio

Mwongozo unatoa taarifa zaidi kuhusiana na kiashiria hiki.

7. Kaya yako ina redio, vifaa vya kaseti/ kanda, au vifaa vyovyote vya hi-fi?
    A. La
    B. Ndio

Mwongozo unatoa taarifa zaidi kuhusiana na kiashiria hiki.

8. Kaya yako ina taa zozote?
    A. La
    B. Ndio

Mwongozo unatoa taarifa zaidi kuhusiana na kiashiria hiki.

9. Kaya yako ina taa meza zozote?
    A. La
    B. Ndio

Mwongozo unatoa taarifa zaidi kuhusiana na kiashiria hiki.

10. Ikiwa kaya ilikuza mimea yoyote katika miezi 12 iliyopita, kwa sasa inamiliki ng'ombe dume, ng'ombe kike, ng'ombe dume aliyehasiwa, mori, ndama wa kiume, ndama wa kike, au ng'ombe maksai wowote?
    A. Hakuna mimea, na hakuna ng'ombe
    B. Hakuna mimea, na ng'ombe wako
    C. Mimea, lakini hakuna ng'ombe
    D. Mimea, na ng'ombe

Kulingana na uk. 16 wa *Mwongozo*, miezi 12 iliyopita ni "miezi 12 iliyopita mpaka siku moja kabla ya mahojiano."

Kulingana na uk. 60 wa *Mwongozo*, tofauti kati ya aina za ng'ombe ni:

- *"Ng'ombe dume*: Ng'ombe wa kiuke aliyekomaa na hajahasiwa anayetumika kwa uzalishaji
- *Ngombe kike:* Ng'ombe wa kike ambaye amezaa angalau mata moja
- *Ng'ombe dume aliyehasiwa:* Ng'ombe wa kiume aliyehasiwa na mwenye umri wa zaidi ya mwaka 1
- *Mori:* Ng'ombe wa kike mwenye umri wa mwaka 1, hadi wakati wa kuzaa ndama wa kwanza
- *Ng'ombe maksai:* Ng'ombe wa kiume aliyehasiwa mwenye umri wa zaidi ya mwaka 1 anayetumiwa kama mnyama wa kazi (kwa mfano, kwa ukulima)
- *Ndama:* Ng'ombe mchanga chini ya umri wa mwaka 1"

Weka alama kwenye jibu mwafaka kimsingi na muunganiko wa ukulima wa mimea na umiliki wa ng'ombe:

Mimea	**Ng'ombe**	**Jibu**
La	La	A
La	Ndio	B
Ndio	La	C
Ndio	Ndio	D

Jedwali la 1: Mistari ya umaskini ya kitaifa, viwango vya umaskini, na kima cha sampuli za Tanzania, Dar es Salaam, Miji mingine, na Vijiji, kwa sampuli za ujenzi na uthibitisho, kwa kaya na watu, kwa mwaka wa 2011/12

	Mstari au Kiwango	Kaya au Watu	Kaya Washiriki	Mistari ya umaskini (TZS kwa mtu mzima kwa siku) na viwango vya umaskini (%)			
					Mistari ya umaskini ya kitaifa		
Eneo				**Chakula**	**100%**	**150%**	**200%**
Tanzania nzima							
	Mstari	Watu		852	1,191	1,787	2,382
	Kiwango	Kaya	10,186	7.2	21.5	32.2	43.0
	Kiwango	Watu		9.7	28.2	42.3	56.3
Dar es Salaam							
	Mstari	Watu		1,019	1,426	2,139	2,852
	Kiwango	Kaya	3,016	0.7	2.6	3.9	5.2
	Kiwango	Watu		1.0	4.1	6.2	8.2
Miji mingine							
	Mstari	Watu		883	2,235	3,352	4,470
	Kiwango	Kaya	3,040	6.0	16.0	24.0	32.0
	Kiwango	Watu		8.7	21.7	32.5	43.4
Vijiji							
	Mstari	Watu		820	1,146	1,719	2,292
	Kiwango	Kaya	4,130	8.8	26.7	40.0	53.4
	Kiwango	Watu		11.3	33.3	49.9	66.6
Ujenzi na Usawazishaji (Kuchagua viashiria na alama, na kuhusisha alama na uwezekano wa umaskini)							
	Kiwango	Kaya	5,109	7.0	21.5	32.2	43.0
Uthibitisho (Usahihi wa kupima)							
	Kiwango	Kaya	5,077	7.2	21.5	32.2	43.0

Chanzo: 2011/12 HBS.

Mistari ya umaskini katika viwango vya kila siku vya TZS kwa mtu mzima katika bei wastani kwa Tanzania nzima wakati wa kazi ya uwandani ya HBS ya 2011/12.

Jedwali la 1: Mistari ya umaskini ya PPP ya mwaka wa 2005 na 2011 ya kimataifa ya kitaifa, viwango vya umaskini, na kima cha sampuli za Tanzania, Dar es Salaam, Miji mingine, na Vijiji, kwa sampuli za ujenzi na uthibitisho, kwa kaya na watu, kwa mwaka wa 2011/12

				Mistari ya umaskini (TZS kwa mtu mzima kwa siku) na viwango vya umaskini (%)							
	Mstari au	Kaya au	Kaya	Mistari ya umaskini ya PPP ya 2005				Mistari ya umaskini ya PPP ya 2011			
Eneo	**Kiwango**	**Watu**	**Washiriki**	**$1.25**	**$2.00**	**$2.50**	**$5.00**	**$1.90**	**$3.10**	**$3.80**	**$4.00**
Tanzania nzima											
	Mstari	Watu		1,139	1,823	2,279	4,557	1,261	1,394	2,523	2,655
	Kiwango	Kaya	10,186	32.2	63.0	74.9	93.7	39.4	69.5	79.0	80.7
	Kiwango	Watu		40.7	72.8	83.2	96.7	49.0	78.6	86.3	87.8
Dar es Salaam											
	Mstari	Watu		1,364	2,182	2,728	5,455	1,510	1,669	3,020	3,179
	Kiwango	Kaya	3,016	4.5	23.1	37.2	78.4	7.5	30.4	43.7	46.9
	Kiwango	Watu		6.9	31.9	48.1	86.0	11.3	40.2	54.9	58.0
Miji mingine											
	Mstari	Watu		1,181	1,890	2,362	4,725	1,308	1,445	2,616	2,753
	Kiwango	Kaya	3,040	22.5	52.1	65.9	90.0	28.6	59.0	70.5	72.8
	Kiwango	Watu		29.7	61.9	74.9	94.2	36.9	68.5	79.1	81.4
Vijiji											
	Mstari	Watu		1,096	1,754	2,193	4,386	1,214	1,342	2,428	2,556
	Kiwango	Kaya	4,130	40.4	73.8	84.7	97.6	48.6	80.0	88.2	89.5
	Kiwango	Watu		48.4	81.5	90.3	98.8	57.5	86.6	92.7	93.7
Ujenzi na Usawazishaji (Kuchagua viashiria na alama, na kuhusisha alama na uwezekano wa umaskini)											
	Kiwango	Kaya	5,109	32.2	62.7	74.9	93.9	39.4	69.3	79.0	80.9
Uthibitisho (Usahihi wa kupima)											
	Kiwango	Kaya	5,077	32.2	63.0	74.9	93.7	39.4	69.5	79.0	80.7

Chanzo: 2011/12 HBS.

Mistari ya umaskini katika viwango vya kila siku vya TZS kwa mtu mmoja katika bei wastani kwa Tanzania nzima wakati wa kazi ya uwandani ya HBS ya 2011/12.

Jedwali la 1: Mistari ya umaskini husiani na yenye msingi wa asilimia ya kitaifa, viwango vya umaskini, na kima cha sampuli za Tanzania, Dar es Salaam, Miji mingine, na Vijiji, kwa sampuli za ujenzi na uthibitisho, kwa kaya na watu, kwa mwaka wa 2011/12

				Mistari ya umaskini (TZS kwa mtu mzima kwa siku) na viwango vya umaskini (%)					
	Mstari au	Kaya au	Kaya	Nusu maskini zaidi	Mistari kwa msingi wa asilimia				
Eneo	**Kiwango**	**Watu**	**Washiriki**	**<100% Kitaifa.**	**Ya 20**	**Ya 40**	**Ya 50**	**Ya 60**	**Ya 80**
Tanzania nzima									
	Mstari	Watu		693	766	1,071	1,225	1,432	2,179
	Kiwango	Kaya	10,186	10.5	14.6	31.4	40.3	49.8	71.6
	Kiwango	Watu		14.1	20.0	40.0	50.0	60.0	80.0
Dar es Salaam									
	Mstari	Watu		829	917	1,281	1,466	1,714	2,608
	Kiwango	Kaya	3,016	0.2	0.3	1.0	1.7	3.2	13.8
	Kiwango	Watu		0.3	0.6	1.7	2.8	4.9	19.6
Miji mingine									
	Mstari	Watu		718	795	1,110	1,270	1,484	2,259
	Kiwango	Kaya	3,040	4.7	6.4	16.7	22.9	32.5	59.3
	Kiwango	Watu		6.7	9.5	22.8	30.1	41.1	69.1
Vijiji									
	Mstari	Watu		667	738	1,030	1,179	1,378	2,097
	Kiwango	Kaya	4,130	14.1	19.8	41.6	52.8	63.8	86.2
	Kiwango	Watu		18.0	25.5	50.0	61.9	72.8	91.4
Ujenzi na Usawazishaji (Kuchagua viashiria na alama, na kuhusisha alama na uwezekano wa umaskini)									
	Kiwango	Kaya	5,109	10.5	14.8	31.6	40.1	49.8	71.4
Uthibitisho (Usahihi wa kupima)									
	Kiwango	Kaya	5,077	10.5	14.6	31.4	40.3	49.8	71.6

Chanzo: 2011/12 HBS.

Mistari ya umaskini katika viwango vya kila siku vya TZS kwa mtu mmoja katika bei wastani kwa Tanzania nzima wakati wa kazi ya uwandani ya HBS ya 2011/12.

Majedwali ya
100% ya Mstari wa Umaskini wa Kitaifa

(na majedwali kuhusu mistari yote ya umaskini)

Jedwali la 3 (100% ya mstari wa kitaifa): Makadirio ya uwezekano wa umaskini yanayohusishwa na alama

Ikiwa alama ya kaya ni . . .	. . . Basi uwezekano (%) wa kuwa chini ya mstari wa umaskini ni:
0–4	100.0
5–9	100.0
10–14	82.3
15–19	62.1
20–24	51.2
25–29	40.3
30–34	32.9
35–39	20.2
40–44	14.0
45–49	10.9
50–54	6.6
55–59	4.1
60–64	2.2
65–69	1.3
70–74	1.0
75–79	1.0
80–84	1.0
85–89	0.0
90–94	0.0
95–100	0.0

Jedwali la 4 (100% ya mstari wa kitaifa): Upatikanaji wa makadirio ya uwezekano wa umaskini yanayohusishwa na alama

Score	Kaya katika kiwango na < mstari wa umaskini		Kaya zote katika kiwango		Uwezekano wa umaskini (%)
0–4	0	÷	0	=	100.0
5–9	202	÷	202	=	100.0
10–14	1,251	÷	1,521	=	82.3
15–19	2,443	÷	3,935	=	62.1
20–24	3,843	÷	7,499	=	51.2
25–29	4,076	÷	10,104	=	40.3
30–34	3,929	÷	11,924	=	32.9
35–39	2,363	÷	11,705	=	20.2
40–44	1,711	÷	12,177	=	14.0
45–49	985	÷	9,027	=	10.9
50–54	537	÷	8,154	=	6.6
55–59	242	÷	5,902	=	4.1
60–64	102	÷	4,593	=	2.2
65–69	70	÷	5,466	=	1.3
70–74	29	÷	2,926	=	1.0
75–79	19	÷	1,922	=	1.0
80–84	19	÷	1,873	=	1.0
85–89	0	÷	1,026	=	0.0
90–94	0	÷	39	=	0.0
95–100	0	÷	6	=	0.0

Idadi ya kaya zote zilizofanywa sawa ili kuwa jumla ya 100,000.

Jedwali la 5 (100% ya mstari wa kitaifa): Hitilafu (tofauti wastani kati ya makadirio na hali halisi ya uwezekano wa umaskini kwa kaya kwa aina ya alama), pamoja na vipindi vya imani, kutokana na hesabu za $n = 16{,}384$, kadi ya alama ya 2011/12 imetumiwa kwa sampuli ya uthibitisho

	Tofauti kati ya kadirio na kiwango halisi			
		Kipindi cha imani (±alama za asilimia)		
Score	**Tofauti**	**Asilimia 90**	**Asilimia 95**	**Asilimia 99**
0–4	0.0	0.0	0.0	0.0
5–9	0.0	0.0	0.0	0.0
10–14	+18.0	5.3	6.4	8.3
15–19	−7.3	5.2	5.5	6.1
20–24	+6.9	2.5	3.0	4.0
25–29	−4.4	3.3	3.5	4.1
30–34	+5.9	1.8	2.2	2.8
35–39	−4.1	2.9	3.1	3.4
40–44	−1.1	1.5	1.8	2.3
45–49	−0.8	1.7	2.0	2.8
50–54	+1.4	1.0	1.2	1.7
55–59	−6.6	4.5	4.7	5.2
60–64	+0.7	0.7	0.9	1.1
65–69	−0.8	0.9	1.1	1.4
70–74	−0.5	0.9	1.1	1.4
75–79	+0.9	0.1	0.1	0.1
80–84	+0.5	0.5	0.6	0.8
85–89	0.0	0.0	0.0	0.0
90–94	0.0	0.0	0.0	0.0
95–100	0.0	0.0	0.0	0.0

Jedwali la 6 (100% ya mstari wa kitaifa): Hitilafu (tofauti wastani kati ya makadirio ya viwango vya umaskini na viwango halisi) kwa kundi kwa wakati fulani kwa kima cha sampuli, pamoja na vipindi vya imani, kwa hesabu 1000 za vima mbalimbali vya sampuli, kadi ya alama ya 2011/12 imetumiwa kwa sampuli ya uthibitisho

Sampuli ya kima	Tofauti kati ya kadirio na kiwango halisi			
		Kipindi cha imani (±alama za asilimia)		
n	Tofauti	Asilimia 90	Asilimia 95	Asilimia 99
1	+0.1	65.5	68.6	79.0
4	–0.9	36.1	41.3	55.1
8	–0.5	28.5	32.7	41.5
16	–0.2	19.7	23.1	28.9
32	+0.1	14.4	16.3	20.8
64	0.0	10.3	11.9	15.1
128	+0.1	7.0	8.4	11.2
256	–0.1	5.2	6.0	7.9
512	–0.1	3.6	4.4	5.9
1,024	–0.1	2.5	3.0	4.1
2,048	0.0	1.8	2.1	2.8
4,096	0.0	1.3	1.5	2.0
8,192	0.0	0.9	1.1	1.5
16,384	0.0	0.7	0.8	1.0

Jedwali la 7 (Mistari ya umaskini ya kitaifa): Hitilafu (tofauti wastani kati ya makadirio na viwango halisi) kwa viwango vya umaskini vilivyokadiriwa vya kundi la kaya, katika wakati fulani, usahihi, na kipengele cha α cha usahihi, kadi ya alama ya 2011/12 imetumiwa kwa sampuli ya uthibitisho

	Mistari ya umaskini			
		Mistari ya umaskini ya kitaifa		
	Chakula	**100%**	**150%**	**200%**
Hitilafu (kadirio uondoe kiwango halisi)	–1.0	0.0	–0.2	+0.4
Usahihi wa tofauti	0.5	0.7	0.7	0.6
Kipengele cha α cha usahihi	1.42	1.20	1.04	0.95

Matokeo yanahusu kadi ya alama ya 2011/12 iliyotumiwa kwa sampuli ya uthibitisho ya 2011/12.

Hitilafu (tofauti kati ya makadirio na viwango halisi) zinaonyeshwa kwa viwango vya alama za asilimia.

Usahihi unapimwa kama vipindi vya imani vya asilimia 90 vya makadirio kwa viwango vya ± alama za asilimia.

Hitilafu na usahihi uliokadiriwa kutokana na hesabu 1,000 zikitumia $n = 16{,}384$.

α imekadiriwa kutokana na sampuli 1,000 za hesabu za $n = 256$, 512, 1,024, 2,048, 4,096, 8,192, na 16,384.

Jedwali la 7 (Mistari ya umaskini ya PPP ya mwaka wa 2005 na 2011 ya kimataifa): Hitilafu (tofauti wastani kati ya makadirio na viwango halisi) kwa viwango vya umaskini vilivyokadiriwa vya kundi la kaya, katika wakati fulani, usahihi, na kipengele cha α cha usahihi, kadi ya alama ya 2011/12 imetumiwa kwa sampuli ya uthibitisho

	Mistari ya umaskini							
	Mistari ya umaskini ya PPP ya 2005				Mistari ya umaskini ya PPP ya 2011			
	$1.25	**$2.00**	**$2.50**	**$5.00**	**$1.90**	**$3.10**	**$3.80**	**$4.00**
Hitilafu (kadirio uondoe kiwango halisi)	–0.1	–0.8	0.0	+0.2	0.0	–0.2	–0.1	+0.1
Usahihi wa tofauti	0.7	0.6	0.5	0.2	0.7	0.5	0.5	0.4
Kipengele cha α cha usahihi	1.10	0.94	0.91	0.70	1.05	0.90	0.88	0.84

Matokeo yanahusu kadi ya alama ya 2011/12 iliyotumiwa kwa sampuli ya uthibitisho ya 2011/12.

Hitilafu (tofauti kati ya makadirio na viwango halisi) zinaonyeshwa kwa viwango vya alama za asilimia.

Usahihi unapimwa kama vipindi vya imani vya asilimia 90 vya makadirio kwa viwango vya ± alama za asilimia.

Hitilafu na usahihi uliokadiriwa kutokana na hesabu 1,000 zikitumia n = 16,384.

α imekadiriwa kutokana na sampuli 1,000 za hesabu za n = 256, 512, 1,024, 2,048, 4,096, 8,192, na 16,384.

Jedwali la 7 (Mistari ya umaskini husiani na yenye msingi wa asilimia): Hitilafu (tofauti wastani kati ya makadirio na viwango halisi) kwa viwango vya umaskini vilivyokadiriwa vya kundi la kaya, katika wakati fulani, usahihi, na kipengele cha α cha usahihi, kadi ya alama ya 2011/12 imetumiwa kwa sampuli ya uthibitisho

	Mistari ya umaskini					
	Nusu maskini zaidi	Percentile-based lines				
	<100% Natl.	Ya 20	Ya 40	Ya 50	Ya 60	Ya 80
Hitilafu (kadirio uondoe kiwango halisi)	–0.5	+0.2	–0.3	–1.3	–1.3	–1.8
Usahihi wa tofauti	0.5	0.6	0.7	0.7	0.6	0.5
Kipengele cha α cha usahihi	1.30	1.23	1.09	1.04	0.99	0.86

Matokeo yanahusu kadi ya alama ya 2011/12 iliyotumiwa kwa sampuli ya uthibitisho ya 2011/12.

Hitilafu (tofauti kati ya makadirio na viwango halisi) zinaonyeshwa kwa viwango vya alama za asilimia.

Usahihi unapimwa kama vipindi vya imani vya asilimia 90 vya makadirio kwa viwango vya ± alama za asilimia.

Hitilafu na usahihi uliokadiriwa kutokana na hesabu 1,000 zikitumia n = 16,384.

α imekadiriwa kutokana na sampuli 1,000 za hesabu za n = 256, 512, 1,024, 2,048, 4,096, 8,192, na 16,384.

Jedwali la 8 (Mistari yote ya umaskini): Matokeo ya kulengwa inayowezekana

		Sehemu ya kulenga	
		Lengwa	**Wasiolengwa**
Hali halisi ya umaskini	**Chini ya mstari wa umaskini**	**Kujumuishwa** Chini ya mstari wa umaskini sahihi lengwa	**Kutohusishwa kikamilifu** Chini ya mstari wa umaskini kimakosa wasiolengwa
	Juu ya mstari wa umaskini	**Uvujaji** Juu ya mstari wa umaskini kimakosa lengwa	**Kutojumuishwa** Juu ya mstari wa umaskini sahihi wasiolengwa

Jedwali la 9 (100% ya mstari wa kitaifa): Asilimia za kaya kwa alama ya mchujo na ainisho lengwa, pamoja na kiwango cha marudio na BPAC, kadi ya alama ya 2011/12 imetumiwa kwa sampuli ya uthibitisho

Score	Kujumishwa < mstari wa umaskini kwa usahihi imelengwa	Kutoshiriki Kikamilifu < mstari wa umaskini kimakosa haijalengwa	Uvujaji ? mstari wa umaskini kimakosa imelengwa	Kutojumuishwa ? mstari wa umaskini kwa usahihi haijalengwa	Kiwango cha kushiriki Kujumuishwa + Kutojumuishwa	BPAC Tazama maandishi
?4	0.0	21.5	0.0	78.5	78.5	–100.0
?9	0.2	21.3	0.0	78.5	78.7	–98.1
?14	1.2	20.3	0.5	78.0	79.2	–86.3
?19	3.9	17.6	1.8	76.7	80.6	–55.7
?24	7.1	14.4	6.1	72.4	79.5	–5.8
?29	11.5	10.0	11.7	66.8	78.3	+45.4
?34	15.0	6.5	20.2	58.3	73.2	+5.8
?39	17.6	3.9	29.3	49.2	66.8	–36.4
?44	19.3	2.2	39.8	38.8	58.1	–85.1
?49	20.3	1.2	47.8	30.7	51.0	–122.6
?54	20.8	0.7	55.5	23.0	43.8	–158.2
?59	21.2	0.3	61.0	17.6	38.7	–183.8
?64	21.3	0.2	65.5	13.1	34.3	–204.7
?69	21.4	0.1	70.8	7.7	29.1	–229.6
?74	21.5	0.0	73.7	4.8	26.3	–243.0
?79	21.5	0.0	75.6	2.9	24.4	–251.9
?84	21.5	0.0	77.4	1.1	22.6	–260.5
?89	21.5	0.0	78.5	0.0	21.5	–265.3
?94	21.5	0.0	78.5	0.0	21.5	–265.5
?100	21.5	0.0	78.5	0.0	21.5	–265.5

Kujumuishwa, kutoshiriki kikamilifu, uvujaji, na kutojumuishwa zimefanywa sawa ili kuwa jumla ya 100.

Jedwali la 10 (100% ya mstari wa kitaifa): Mgao wa kaya zote zinazolengwa (yaani, alama katika au chini ya mchujo), mgao wa kaya lengwa ambazo ni maskini (yaani, ina matumizi chini ya mstari wa umaskini), mgao wa kaya maskini ambazo zimelengwa, na idadi ya kaya maskini ambazo zililengwa kwa mafanikio (ujumuishaji) kwa kila kaya ambayo sio maskini lakini ililengwa kimakosa (uvujaji), kadi ya alama ya 2011/12 imetumiwa kwa sampuli ya uthibitisho

Mkato wa kulenga	% ya kaya zote zilizolengwa	% ya kaya zilizolengwa ambazo ni maskini	% ya kaya maskini zilizolengwa	Kaya maskini zilizolengwa kwa kila kaya isio maskini iliyolengwa
?4	0.0	100.0	0.0	Maskini tu zililengwa
?9	0.2	100.0	0.9	Maskini tu zililengwa
?14	1.7	71.0	5.7	2.4:1
?19	5.7	68.2	18.0	2.1:1
?24	13.2	53.8	32.9	1.2:1
?29	23.3	49.5	53.6	1.0:1
?34	35.2	42.5	69.6	0.7:1
?39	46.9	37.5	81.9	0.6:1
?44	59.1	32.7	89.9	0.5:1
?49	68.1	29.8	94.3	0.4:1
?54	76.2	27.3	96.7	0.4:1
?59	82.1	25.8	98.6	0.3:1
?64	86.7	24.5	99.1	0.3:1
?69	92.2	23.2	99.7	0.3:1
?74	95.1	22.6	99.9	0.3:1
?79	97.1	22.1	99.9	0.3:1
?84	98.9	21.7	100.0	0.3:1
?89	100.0	21.5	100.0	0.3:1
?94	100.0	21.5	100.0	0.3:1
?100	100.0	21.5	100.0	0.3:1

Majedwali ya
Mstari wa Umaskini wa Chakula

Jedwali la 3 (Mstari wa umaskini wa chakula): Makadirio ya uwezekano wa umaskini yanayohusishwa na alama

Ikiwa alama ya kaya ni . . .	. . . Basi uwezekano (%) wa kuwa chini ya mstari wa umaskini ni:
0–4	100.0
5–9	39.5
10–14	36.6
15–19	29.9
20–24	21.0
25–29	13.3
30–34	10.4
35–39	4.4
40–44	2.8
45–49	1.5
50–54	1.3
55–59	0.6
60–64	0.6
65–69	0.4
70–74	0.0
75–79	0.0
80–84	0.0
85–89	0.0
90–94	0.0
95–100	0.0

Jedwali la 5 (Mstari wa umaskini wa chakula): Hitilafu (tofauti wastani kati ya makadirio na hali halisi ya uwezekano wa umaskini kwa kaya kwa aina ya alama), pamoja na vipindi vya imani, kutokana na hesabu za n = 16,384, kadi ya alama ya 2011/12 imetumiwa kwa sampuli ya uthibitisho

	Tofauti kati ya kadirio na kiwango halisi			
		Kipindi cha imani (±alama za asilimia)		
Score	**Tofauti**	**Asilimia 90**	**Asilimia 95**	**Asilimia 99**
0–4	0.0	0.0	0.0	0.0
5–9	–26.6	20.0	21.0	22.2
10–14	+4.9	5.1	6.2	8.5
15–19	–4.4	3.9	4.2	5.2
20–24	+3.5	2.2	2.6	3.3
25–29	–3.8	2.8	3.1	3.4
30–34	+2.1	1.0	1.2	1.7
35–39	–3.4	2.3	2.5	2.7
40–44	–2.2	1.7	1.9	2.1
45–49	+0.7	0.3	0.4	0.6
50–54	–0.5	0.6	0.7	1.0
55–59	–4.5	3.3	3.5	4.0
60–64	+0.4	0.2	0.2	0.3
65–69	–0.8	0.9	1.0	1.2
70–74	–0.9	0.9	1.0	1.3
75–79	0.0	0.0	0.0	0.0
80–84	0.0	0.0	0.0	0.0
85–89	0.0	0.0	0.0	0.0
90–94	0.0	0.0	0.0	0.0
95–100	0.0	0.0	0.0	0.0

